

# Kushurulikia Mutu Unafikili kuwa na Ebola:

# KUWA ANGALIFU (PRUDENT) UNAPOONGOJA




# Kushurulikia Mutu Unafikili kuwa na Ebola: Kuwa Angalifu (prudent) Unapoongoja 1







Ikiwa mupendwa wako ni mugonjwa na unafikili ni Ebola, piga simu ili upate usaidizi. Usimuguze, damu yake ao maji ya mwili yake (matapiko, mavi, mkojo, jasho). Umwambie akunywe SRO mingi ao maji. Wagonjwa wanaokunywa SRO mingi mapema wanakuwa na bahati sana ya kuishi.

# Kushurulikia Mutu Unafikili kuwa na Ebola: Kuwa Angalifu (prudent) Unapoongoja 2






Inafaa mutu mumoja tu ashurulikie mugonjwa unapoongoja usaidizi. Usiwaruhusu wale watu wengine ya jamaa wakaribie ao kusaidia. Kaa mbali na mgonjwa fkama metre 1. Usiguzee kopo ile mugonjwa anatumia. Jaza chupa tena bila kuishika. Usiguzee nguo za kitanda, draps ao vitu vingine mugonjwa aliguza alipokuwa mugonjwa.

# Kushurulikia Mutu Unafikili kuwa na Ebola: Kuwa Angalifu (prudent) Unapoongoja 3



CS295757-C Swahili



Unaposhurulikia mugonjwa wako,usimuguze, na nawa mikono yako mara mingi ukitumia sabuni na maji ao muchanganyiko ya chlore, hata kama haujamuguza. Vaa vizuizi vya kujikinga kama vile gants na ufunike kila sehemu ya ngozi zile hazijafunikwa. Nawa mikono kila wakati unapotoa usaidizi.

# Kushurulikia Mutu Unafikili kuwa na Ebola: Kuwa Angalifu (prudent) Unapoongoja 4



# Kushurulikia Mutu Unafikili kuwa na Ebola: Kuwa Angalifu (prudent) Unapoongoja 4




Inafaa wagonjwa wale unafikili wanakuwa na Ebola washurulikiwe katika pahali pa matunzo. Ikiwa mupendwa wako ni mugonjwa, ana nafasi nzuri zaidi ya kuishi kupitia utunzaji katika pahali pa matunzo. Hii inasaidia pya kulinda jamaa yako.